



**OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**



---

## SHULE YA MSINGI IDINDILIMUNYO

### TANGAZO LA KUMPATA MSIMAMIZI WA MRADI MWENYE FANI YA UJENZI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA PROGRAMU YA BOOST

TAREHE 12/5/2023

Shule ya Msingi Idindilimunyo imepokea fedha kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule kwa programu ya BOOST ambayo ni ujenzi wa Madarasa matatu (3). Aidha kwa mujibu wa muongozo kazi hizi zitasimamiwa na mtaalamu/wataalamu wenye ujuzi, uzoefu na wenye taaluma ya ufundi kwa kazi za ujenzi.

1. Hivyo, wataalamu wote wenye ujuzi, uzoefu na wenye taaluma ya ufundi kwa kazi za ujenzi ndani ya mradi au nje ya mradi wanaalikwa kutuma maombi yao kupitia kwa wasimamizi waliokasimishwa madaraka ya afisa masuhuli katika ngazi ya vituo ambapo katika shule ni mwalimu Mkuu kuanzia tarehe 12/5/2023
2. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni tarehe 17/5/2023 **saa 7:30 mchana**. Kotesheni zote zitafunguliwa kwa uwazi mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.

Kotesheni zote lazima zijazwe kikamilifu na kufungwa kwenye bahasha na kuwasilishwa, kupitia..anwani **ifuatayo Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi Idindilimunyo S.L.P 66 Njome**

3. Kotesheni zitakazochelewa na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa.

4.

#### **Jedwali la miundombinu itakayojengwa**

<b>Na</b>	<b>AINA YA KAZI</b>	<b>NAMBA YA ZABUNI</b>
1	Ujenzi Wa Madarasa Matatu (3)	<b>LGA/153/2022/2023/W/17</b>

#### **KAZI ANAZOTAKIWA KUFANYA FUNDI**

- .A.Msingi wa jengo (substructure )
- B.Kunyanyua Jengo (Super structure)
- C.Kuezeka (Roof structure and covering )
- D.Milango
- E.Umaliziaji (Finishing)
- F.Rangi na Mapambo (Painting and Decoration)
- G.Umeme (Electrical installation )
- H.Mifumo ya maji

#### **SIFA ZA WAOMBAJI**

- Waombaji wote lazima wawe na taaluma ya ujenzi kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali katika ngazi ya fundi stadi(VETA daraja la I),Fundi sanifu ngazi ya FTC/Diploma au Shahada
- Uzoefu wa kujenga/kusimamia majengo ya serikali au taasisi kwa muda usiopungua miaka 3
- Ujuzi wa kutafsiri michoro na mchanganuo wa vifaa(schedule of materials)
- Uwezo wa kujisimamia,kusimamia kundi kubwa mafundi na vibarua kwa kuwapangia kazi kwa ukubwa unaostahili(piece work)
- Uwezo wa kuandaa mpango kazi(Working programme)

#### **MAJUKUMU**

- Kusimamia kundi kubwa mafundi na vibarua kwa kuwapangia kazi kwa ukubwa unaostahili(piece work)
- Kupima kazi iliyofanywa na mafundi waliopo chini yake kwaajili ya kuombewa malipo
- Kusimamia ubora wa kazi kwaniaba ya mwajiri chini ya Mhandisi wa Ujenzi/Miundombinu(W)
- Kuandaa mpango kazi(Working programme)
- Kuandaa taarifa ya mradi hatua kwa hatua
- Kuandaa malipo kwaajili ya mafundi wa fani tofaauti na vibarua waliopo chini yako
- Kusimamia matumizi ya vifaa vifaa vya mwajiri

- Kutoa taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa kamati za usimamizi wa mradi
- Kutoa ushauri kwa mwajiri kabla ya kutekelezaji ili ushauri huo ujadiliwe
- Kutunza daftari la kutunza vifaa(site ledger)
- Kutunza daftari la mahudhurio kwa mafundi na vibarua
- Kukaa kwenye eneo la mradi muda wote wa utekelezaji
- Kushirikiana na kamati za mradi kusimamia utendaji

### **MASHARTI YA UJUMLA**

- Awe raia wa Tanzania
- Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea
- Asiwe mwajiriwa wa serikali
- Awe hajawahi kushtakiwa
- Aambatishe cheti cha NIDA
- Awe na barua ya utambulisho toka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kata

**Tanbihi:** Mafundi wengine wa fani mbalimbali (uashi, useremala, ucholemeaji, rangi, umeme n.k) watakaosimamiwa na msimamizi mkuu watatuma maombi yao moja kwa moja wakati wa utekelezaji wa mradi eneo la mradi

Fomu ya kujaza gharama za usimamizi (supervision), mafundi na vibarua (schedule of labour) inapatikana kwa **Mwalimu mkuu shule ya msingi Idindilimunyo** kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa

**Limetolewa na:** Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi Idindilimunyo.

**S.L.P 66 NJIMBE**

.....  
 FELIO EBEHARD NJOGOPA  
 MWALIMU MKUU